


Unazijua?
Fanya
jaribio!

**KUHUSU KIJITABU HIKI:** Umekisoma kitabu kilichouzwa zaidi hapa duniani – *BIBLIA TAKATIFU* – Kitabu kilicho na yaliyopita, yaliyopo na yajayo kuhusu wanadamu? Biblia huchukua masaa kama 70 kuisoma. *HABARI ZAKO* hujumuisha habari na ujumbe wake wa ajabu.

*"Pokea* ***mafundisho*** *yangu, wala si* ***fedha,***
*Na* ***maarifa*** *kuliko* ***dhahabu*** *safi.*
*Maana* ***hekima*** *ni bora kuliko* ***marijani;***
*Wala vyote vinavyotamanika havilingani nayo."*
**Muumbaji wako** (Mithali 8: 10-11)

**KUHUSU MWANDISHI WAKE:** P.D. Bramsen ametumia muda mwingi wa maisha yake huko Senegal, taifa lenye Waislamu wengi kwenye ukingo wa Sahara. Maandishi yake hutokana na upendo wake kwa Maandiko na maelfu ya mahojiano na marafiki wa Kiisllamu wa Senegal na sehemu nyingi duniani.

# UNAZIIJUA VEMA KIASI GANI HABARI ZAKO?

**1.** Wazazi wako wanaitwaje?


**2.** Wazazi wa wazazi wako wanaitwaje?

**3.** Wazazi wa wazazi wa wazazi wako wanaitwaje?

**4.** Wazazi wa wazazi wa wazazi wa wazazi wa wazazi wa wazazi wa wazazi wa wazazi wa wazazi wako wanaitwaje? (Wamefika 512!)

Ukipewa dhahabu yote duniani – utayatambua majina ya kila mmoja wa wazazi wako wa vizazi 10 vilivyopita? Huenda hutaweza! Kwa sababu *huna kumbukumbu ya maandishi* ya uzao wako wa kipindi kirefu kama hicho.

Sasa fikiria eneo la zamani zaidi la habari zako – kipande cha historia chenye dhamani kuliko dhahabu yote ya ulimwengu.



**Wazazi wako wa kwanza.** Unazijua habari zao? Bila ya *kumbukumbu ya maandishi* ya habari zao, hungejua ulikotoka au kwa nini upo hapa. Cha kushukuru ni kuwa ipo *kumbukumbu hiyo.*


**Unajua inasemaje?**

## Kumbukumbu



**K****itabu** kiitwacho *Biblia Takatifu** si tu kinauzwa zaidi na kimetafsiriwa zaidi kuliko kitabu kingine duniani na pia ndiyo maandiko ya kale yaliyohifadhiwa kuliko mengine*. Biblia, inayodai kuwa ni *Neno la Mungu,* ina sehemu mbili:

Sehemu ya 1: Agano la Kale (Torati, Zaburi, n.k.) – *Mpango wa Mungu Ukitabiriwa*
Sehemu ya 2: Agano Jipya (Injili, n.k.) – *Mpango wa Mungu Ukitimizwa*




**Lakini tutajuaje kama maandiko haya kweli ni kumbukumbu *ya Mungu*?**

Tunaweza kujua kwa sababu yana ushahidi usiopatikana kwenye kitabu kingine, kama vile:

- **Uthabiti kamili.** Maandiko yaliandikwa na makumi ya manabii ndani ya miaka zaidi ya 1500, huku yakifanya ujumbe mmoja ulioungana. Mwandishi pekee asiyethibitiwa na wakati ndiye angeweza kuuvuvia.
- **Habari yenyewe.** Hakuna mwanadamu ambaye angeweza kufikiria historia yenye mambo kama hayo tena mengi hivyo. Vipengele vyake vyote hukaa pamoja kikamilifu. Hujibu maswali makubwa ya maisha, hutoa tumaini, na hubadilisha maisha.
- **Mamia ya unabii uliotimia.** Ni Mungu peke yake awezaye kuifunua historia kabla haijatokea.

*Mtakatifu maana yake ni – *Wa pekee, amewekwa kando, halinganishwi.* Biblia ni neno la Kigiriki lenye maana ya *kitabu* au *maktaba.*
*Kwa maelezo zaidi kuhusu madai ya kijitabu hiki tembelea: **www.one-god.one.message.com**




**Habari zako** zinaanza na *Mungu*. Wakati mwanadamu akiwa na dhana nyingi kuhusu asili ya wazazi wako wa kwanza, kitabu cha Mwanzo (wenye maana ya *asili* ) ni kumbukumbu ya yule aliyekuwako wakati yote yanaanza.

***"Hapo mwanzo Mungu** aliziumba mbingu na nchi."* (Mwanzo 1:1, Torati)

**Kuna Mungu?** Viumbe wake hulijibu swali hili kwa ushawishi wenye hanikizo.

*"Yeye hutandaza kaskazi juu ya nafasi isiyo na kitu."* (Nabii Ayubu, 26:7)

*"Anga huitangaza kazi ya mikono yake."* (Nabii Daudi, zaburi 19:1)



Tukizungumzia mikono, angalia mikono yako mwenyewe. Nani isipokuwa fundi stadi mkuu anayeweza kubuni vifaa kama hivyo? Na ni hekima ya aina gani inayohitajika kutengeneza seli hai yenye mamilioni ya sehemu zinazofanya kazi? Au kufuma pamoja ncha ya kemikali, isiyoonekana bila darubini, yenye urefu uliozungushwa wa mita mbili, yenye mabilioni ya mfumo wa kinasaba unaokufanya wewe uwe *ulivyo*?

*"Ee BWANA…..Uliniumba tumboni mwa mama yangu. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa Kwa jinsi ya ajabu ya kutisha!"* (Zaburi 139:1, 13 – 14)

## Muumbaji wako

**Mungu anafanana na nini?** Yeye ni Mwanzilishi asiyepimika na Muumbaji wa ulimwengu. Hana mwanzo wala mwisho. Yeye ni "*Baba wa roho*" (Waebrania 12:9) aliyewaumba malaika mbinguni na mababa zako wa kwanza wamjue, wampende, wamwabudu na kumtumikia Yeye milele. Mungu ni Mmoja, hata hivyo anaweza kuwa kila mahali kwa wakati mmoja. Jina lake ni *Mweza wa yote,* ambaye kwa *Neno lake* na *Roho wake,* alitamka, ulimwengu ukaonekana.



*"Hapo mwanzo **Mungu** aliziumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; **Roho ya Mungu** ikatulia juu ya uso wa maji. **Mungu akasema,** Iwe nuru; ikawa nuru**.** Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akaitenga nuru na giza."* (Mwanzo 1:1-4)

Siku ya kwanza ya uumbaji, utukufu wa Mungu mwenyewe uliyamulika mandhari. ***"Mungu ni nuru,*** *wala giza lo lote hamna ndani yake. Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli."* (1Yohana 1:5-6) Muumbaji wako ni mkamilifu. Ni viumbe wasafi kikamilifu pekee wanaoweza kuishi naye. ***"Mungu wetu ndiye mtakatifu."*** (Zaburi 99:9)

Katika siku sita za kiutaratibu wa Mungu, Mungu aliye nuru aliumba anga, nchi, bahari, mimea, jua, mwezi, nyota, samaki, ndege, wadudu, na wanyama. Ni sayari ya ajabu! Ingetawaliwa vizuri, Dunia haingepungukiwa na cho chote chema. Ingekuwa makao yafaayo kwa wanadamu.

*"Mungu akasema, 'na tumfanye* mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale...nchi yote pia...' Mungu akaumba mtu...**kwa mfano wa Mungu**...mwanamume na mwanamke aliwaumba."* (Mwanzo 1:26-27)

Tofauti na wanyama, wanadamu waliumbwa waonyeshe asili ya muumbaji wao. Mungu aliwapa nafsi za milele, akili yenye nguvu, hisia yenye kina, na uwezo wa kufanya maamuzi yenye matokeo ya kudumu milele. Mungu hakupenda roboti. Alitaka wazazi wako wa kwanza, Adamu na Hawa, kukuza uhusiano, siyo tu wao kwa wao, bali pia pamoja naye. Anatamani kile kile kwa ajili yako. ***"Mungu ni upendo."*** (1Yohana 4:8)

*Kwa kuwa Mungu ni MMOJA, kwa nini anasema, *"Na TUmfanye mtu kwa mfano WETU. . ."?* Jibu limefunikwa kwenye umoja wake wenye wingi. Kwenye maandiko, neno la Kiebrania lenye maana ya *"Mungu"* ni *Elohim,* ambayo ni *nomino yenye wingi.* Neno linalotumika kwa *"mmoja"* ni *echad* lenye maana ya *umoja wenye wingi.* Kwenye umilele, kabla ya kuumba malaika au mwanadamu, Mungu alifurahia uhusiano wa upendo na mawasiliano ndani yake Yeye mwenyewe – na Neno lake yeye binafsi – na Roho wake Mtakatifu. *"Mungu ni mkuu – nasi hatumjui!"* (Nabii Ayubu 36:26)


## Sheria ya Dhambi na Mauti

Hapo mwanzo, Mungu na mwanadamu walikuwa marafiki. Lakini Mungu alipanga kuujaribu urafiki huo, akiwapa Adamu na Hawa nafasi ya kuuboresha uhusiano wao na Muumbaji wao kwa kumwamini na kumtii. Na hivyo, hata kabla BWANA Mungu hajamuumba Hawa, alimweka Adamu kwenye bustani kamilifu yenye mandhari mazuri na sauti nzuri, wanyama wa kipekee, na miti yote ya matunda alipewa aweze kula – lakini alipewa sharti moja.

*"BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, `**Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula,** walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana **siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.'"*** (Mwanzo 2:16-17)

Matokeo ya kutotii agizo moja la Mungu yangekuwaje?

Mungu alimwambia adamu kuwa akila tunda alilokatazwa lazima aanze kutumia shanga za sala, aombe, afunge, atoe sadaka, ahudhurie mikusanyiko ya kidini, na kutenda matendo mema "kuleta uwiano" wa matendo yake mabaya kisha atumainie huruma ya Mungu? Mungu alisema hivyo? **Hapana!!!**



Mungu alimwambia Adamu kuwa DHAMBI lazima ilipwe kwa **KIFO**. Biblia huiita hii ***"sheria ya dhambi na mauti"*** (Warumi 8:2)

Sheria hii ya kwanza aliyopewa mwanadamu na Muumba wake inatoa ufunguo wa kuzielewa habari zako – zilizopita, za sasa, na zijazo.

**Dhambi** (kuivunja sheria ya Mungu) husababisha **kutengana kwa aina tatu:**

1. **Kifo cha roho** – roho ya mwanadamu kutengana na Mungu.
2. **Kifo cha mwili** – nafsi kutengana na mwili.
3. **Kifo cha milele** – mwanadamu kutengana na Mungu milele motoni, "*moto wa milele, aliowekewa tayari ibilisi na malaika zake*". (Mathayo 25:41)

Maana ya kifo inaweza kufanyiwa kielelezo na tawi la mti. Tawi hai la mti linapovunjwa, ingawa bado linaonekana kuwa hai, "limekufa" kwa kuwa limetenganishwa na chanzo chake cha uhai.



Mungu alikuwa akimwonya Adamu kuwa **dhambi ingemtenganisha** na Muumba wake aliye Chanzo cha Uhai. Kwa Mungu aliye mkamilifu na mtakatifu, dhambi si jambo dogo.

## Uchaguzi


Baada ya BWANA kumuumba mwanamke mzuri kutoka kwenye ubavu wa Adamu, kumkabidhi Adamu na kutangaza kuwa hao ni mume na mke, *"Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni* ***chema sana. . .*** *Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala* ***hawakuona haya."*** (Mwanzo 1:31; 2:25) Fikiria ulimwengu usio na kasoro ukikaliwa na wanandoa wasio na kasoro kwenye uhusiano mzuri na Muumbaji wao asiye na kasoro. Ndivyo mambo yalivyokuwa hapo mwanzo. Bila kasoro. **Basi lilitokea tatizo gani?**

Siku moja, Adamu na Hawa walipokuwa karibu na mti waliokatazwa kula matunda yake, Shetani* alitokea kwa mfano wa nyoka, "*Akamwambia Hawa*, ***Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu,*** *msile matunda ya miti yote ya bustani?* Shetani alitaka wawe na mashaka na neno la Mungu, alimwambia Hawa, ***Hakika hamtakufa****, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."* (Mwanzo 3:1, 4-5) Angalia shetani anavyochanganya kweli na uongo. Mithali ya Kiarabu inasema: "Jihadhari, baadhi ya waongo huitamka kweli!" Huyo mwongo mkuu alitamka uongo akisema, "*Hakika hamtakufa"* na akatamka kweli akisema, mtajua *"mema na mabaya."* Lakini hakuyatamka madhara ya kuogofya yatakayozaliwa na dhambi yao.

*Shetani (yaani *Adui*) mwanzoni alikuwa malaika mbinguni, alitupwa alipojaribu kuwafanya malaika wengine wamwabudu yeye badala ya BWANA. Malaika waliojiunga na uasi wa shetani huitwa *mapepo.*

Muda ukawa umefika wa Adamu na Hawa kuchagua kati ya neno la Mungu na neno la Shetani. Walichagua la Shetani. *Mke alikula,* ***Mume alikula.***

***"Wakafumbuliwa*** *macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi;* ***wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo.*** *Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe* ***wakajificha*** *kati ya miti ya bustani, BWANA Mungu asiwaone. BWANA Mungu akamwita Adamu, akamwambia, '****Uko wapi?'*** *Akasema, Nalisikia sauti yako Bustanini,* ***nikaogopa*** *kwa kuwa mimi ni uchi;* ***nikajificha.'"*** (Mwanzo 3:7-10)



Kwa nini waaibike na kujificha?

Walikuwa wametenda dhambi.

Urafiki wa karibu na Muumbaji wao haupo tena.

Kimwili wahenga wetu walikuwa bado hai lakini kiroho walikuwa **wamekufa.**

## Mungu aliye Mtakatifu

Kabla hawajatenda dhambi, Adamu na Hawa walikuwa wamezungukwa na ukamilifu na utukufu wa Mungu. Walikuwa na **starehe** kamili kwenye uwepo wa Muumba wao, aliyekuja bustanini kutembea na kuzungumza nao. Lakini walipoasi agizo lake **walikosa starehe** kwenye uwepo wake – siyo tu kwa sababu ya uchi wao wa kimwili, bali pia uchi wao wa kiroho.

Kabla hawajakosa walikuwa na **hisia ya Mungu** na *"hawakuona haya."* (Mwanzo 2:25) Sasa wakawa na hisia binafsi na kujisikia wachafu mbele za Mungu.

Walikuwa kinyume na Muumba wao, aliye **mtakatifu.** Sasa walikuwa **waovu.** Hawakutaka tena kuwa kwenye usafi na mng`ao wa uwepo wa Mungu. Kama mende wanaotafuta pa kujificha nuru inapoangaza, sasa *"wakapenda giza kuliko nuru; kwa maana matendo yao yalikuwa maovu."* (Yohana 3:19)


Mungu aliye mkamilifu safi na mtakatifu hawezi kuvumilia dhambi. Walilijua hilo. Je wewe?

Dhambi humchukiza Mungu kama utakavyoona nguruwe aliyeoza nyumbani mwako.

***"Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu,** ni BWANA!"* (Nabii Isaya 6:3)

Mara wazazi wetu wa kwanza walipotenda dhambi, walikuwa kama tawi lililovunjika. *Walijitenga na Mungu,* chanzo cha uhai. Na kama tawi lililotengwa, *miili yao ilianza kufa.* Na bila ya Bwana Mungu kuwakomboa, walikabili *kutengwa milele na Mungu kwenye "ziwa la moto"* (Ufunuo 20:14-15) ambako nafsi zilizoambukizwa dhambi zimezuiliwa milele bila tumaini na kuokoka. Adamu na Hawa walikuwa **wenye dhambi wasio na msaada.** Lakini habari zinazidi kuwa mbaya.

Kwa kuwa Adamu alikuwa kiongozi wa wanadamu, dhambi yake iliuathiri **uzao wakewote.** Ni kama kila kijiti na jani kwenye tawi lililovunjika linavyoathirika, kadhalika na "tawi" la familia ya Adamu. Wote tunatenda dhambi na tunakufa.




*"**Kwa mtu mmoja** dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo **mauti ikawafikia waatu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi."*** (Warumi 5:12)

**Dhambi** (siyo kansa, njaa, umaskini, au bomu la nyuklia) ni kani yenye uharibifu mkubwa zaidi na ni janga linaloenea zaidi kwenye sayari yetu.

## Laana na Mpango

Dhambi ilileta **laana.** Wazazi wetu wa kwanza na uzao wao wakakabili hali ngumu, maumivu, miiba, njaa, magonjwa, uzee, na kifo.



Wengi wetu tumeizoea hali kama hii kiasi cha kuikubali kama "sehemu ya kawaida ya maisha." Lakini ni jambo la kawaida kwa baraka ya kupata mtoto kuhusisha maumivu makali? Au ua la waridi linalonukia kuzaa miiba mikali? Au walioumbwa kwa mfano wa Mungu kufa na kukabili hukumu? Vipengele kama hivi vinavyoingilia si vya kawaida kwenye ulimwengu huu, ni sawa na viini vya kansa kwenye mwili wa mwenye afya.

Habari njema ni kuwa tangu mwanzo Muumba wetu alikuwa na mpango wa kuokoa. Siku ambapo dhambi iliuharibu uzao wa mwanadamu, Mungu aliwapa Adamu na Hawa dokezo la mpango wake. Kwa wakati wake BWANA amtume duniani **Mwokozi,** *"Uzao wa mwanamke"* (Mwanzo 3:15), wa kuwatengenezea njia Adamu na Hawa na uzao wao, ya kuwaokoa kutoka kwa Shetani, dhambi, kifo na hukumu. Huyu Mkombozi atajulikana kama **Masihi,** *Mteule wa Mungu.*

Kilichofuata, kwa huruma na haki yake, Mungu aliwafanyia jambo la ajabu wale waliomwasi.

*"BWANA Mungu akawafanyia Adamu na mkewe **mavazi ya ngozi, akawavika."*** (Mwanzo 3: 21)

Adamu na Hawa walishona majani ya mtini kama juhudi ya kufunika dhambi na aibu yao. Lakini Mungu alizikataa juhudi zao za kuwafanya wakubalike machoni pake. Badala yake, Mungu alichinja wanyama na kuwafunika Adamu na Hawa kwenye ngozi hizo.

Cha kusikitisha ni kuwa ilibidi wanyama wasio na hatia wafe kwa sababu ya dhambi ya Adamu na Hawa. Mungu alikuwa akionyesha picha ya mpango wake wa kuwaokoa wenye dhambi kutoka kwenye *sheria ya dhambi na mauti.* Damu iliyomwagika ilikuwa mfano wa kile kinachohitajika *kusafisha* **dhambi** ya mwanadamu; ngozi zilikuwa mfano wa kilichohitajika kufunika **aibu** ya mwanadamu. Kuanzia wakati huo mwana-kondoo au mnyama mwingine anayekubalika lazima afe kama *mbadala wa muda* wa mwenye dhambi, hadi wakati wa Mungu kuutoa *mbadala wa kudumu.*

Mungu alitoa **dhabihu ya mwanzo** kwa ajili ya dhambi.
Mungu pia angetoa **dhabihu ya mwisho** kwa ajili ya dhambi.

## Wenye dhambi Wanaabudu

Baada ya onyesho hili na neema (*wema wasioustahili*), Mungu aliwatoa Adamu na Hawa kwenye bustani iliyo kamili hadi kwenye ulimwengu uliolaaniwa kwa sababu ya dhambi. Dhambi yao iliwatenganisha na Mungu. Wazazi wetu wa kwanza walikuwa na tatizo kubwa. Kadhalika na sisi.

Baadaye Hawa alimzaa mtoto wa kwanza duniani, Kaini. Kisha alizaliwa Habili, ndugu yake. Vijana wote wawili walirithi asili ya dhambi ya wazazi wao. Kama mithali za Kiafrika zinavyosema:

- "Panya hazai uzao usiochimba"
- "Madhara ya janga  hayakomei kwa aliyeyaanzisha"

Kama vijana, Kaini na Habili walitaka kumwabudu Muumba wao. Lakini kama walitaka kuwa na uhusiano naye, ilibidi watimize masharti yake: *"pasipo kumwaga damu* (malipo ya kifo) *hakuna ondoleo* (la deni ya dhambi)*."* (Waebrania 9:22)

Kaini alimkaribia Mungu kwa **njia yake mwenyewe.** Alimtolea Mungu mazao aliyolima kwa bidii. Kaini alikuwa kama watu leo wanaojaribu kupata upendeleo kwa Mungu kwa desturi za kidini na matendo mema, wakipuuza ukweli kuwa dhambi malipo yake ni *kifo,* si jitihada ya mtu.  Mungu aliikataa sadaka ya Kaini. Wakati huo Habili alimkaribia Mungu kwa imani katika **njia ya Mungu.** Habili alileta malipo ya kifo – damu ya mwana-kondoo aliyetolewa sadaka.

Mfikirie Habili akiweka mkono wake kwenye kichwa cha mwana-kondoo asiye na hatia na kumshukuru BWANA kuwa ingawa yeye Habili alistahili kifo na kutengwa na Muumbaji wake milele, Mungu angempokea mwana-kondoo kama mbadala wake. Mwana-kondoo (ambaye hakuwa na deni la dhambi) alikufa badala yake.



Habili aliiheshimu sheria ya **dhambi na mauti,** ndiyo sababu *"BWANA akamtakabali habili na sadaka yake; bali Kaini hakumtakabali."* (Mwanzo 4:4-5)

Ingawa Kaini alimkaribia Mungu kimakosa, Mungu bado alimpenda na kumhimiza atubu, yaani, *abadili mawazo yake* na kujikabidhi kwenye njia ya Mungu ya msamaha na haki. Lakini Kaini alikataa kutoa damu ya mwana-kondoo kwa ajili ya dhambi zake. Badala yake, katika hasira yake na kiburi cha kidini, alimwua Habili na kumpa mgongo Mungu.

Maandiko yanatueleza kuwa Adamu na Hawa walizaa na wengine *"waume na wake."* (Mwanzo 5:4) Baadhi walichagua kumtumaini na kumtii Mungu, lakini wengi wao walichagua kufuata njia ya Kaini.


## Imani kwa Mungu na Mpango wake

Vizazi virefu kumi baada ya Adamu, Mungu alitoa ripoti hii mbaya kuhusu mwanadamu:…"*kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote."* (Mwanzo 6:5) Baada ya uvumilivu mkubwa, Mungu aliuhukumu uovu kwa gharika la dunia nzima, akiwasalimisha tu Nuhu na familia yake, waliomwamini BWANA na mpango wake. Mungu pia alisalimisha wawili wawili wa kila mnyama na ndege, wa kiume na wa kike, na saba kwa saba dume kwa jike wa kila mnyama anayefaa kwa sadaka. Na jambo la kwanza kufanya Nuhu baada ya gharika kwisha ni nini? *"Nuhu akamjengea BWANA madhabahu; akatwaa katika kila mnyama aliye safi, na katika kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka ya kuteketezwa juu za madhabahu."* (Mwanzo 8:20)

Pamoja na kubarikiwa uanze upya, uzao wa wanadamu uligeuka na kumwacha Muumba wao. Vizazi kumi baada ya Nuhu Mungu alimwita Abrahamu aiache nyumba na dini ya baba yake, aiweke imani na tumaini kwake peke yake. Maandiko yanasema: *"'Ibrahimu **alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki;'** naye aliitwa rafiki wa Mungu."* (Yakobo 2:23; Mwanzo 15:6) Kwa nini Mungu alimtangaza Ibrahimu kuwa mwenye haki? Kwa sababu Ibrahimu alimwamini Mungu na neno lake. Mungu alimwahidi Ibrahimu, *"Nitakufanya wewe kuwa **taifa kubwa**. . .na **katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."*** (Mwanzo 12:2-3) Mungu aliitunza ahadi yake. Manabii, Maandiko, na Masihi vyote vilikuja kwetu kwa kupitia taifa hilo.

Ibrahimu alipokuwa mzee sana, BWANA alimwagiza kufanya jambo gumu. Alimwambia aende kwenye mlima fulani akajenge madhabahu amtoe mwanawe sadaka! Ibrahimu alitambua kuwa Mungu ni mwenye haki, mwema, na wa kuaminiwa, hivyo alitii.

Siku tatu baadaye, baba na mwana wakipanda mlimani, mwana wa Ibrahimu aliuliza, *"Babangu!..**yuko wapi mwana-kondoo** wa sadaka ya kuteketezwa?" Ibrahimu akasema, `**Mungu atajipatia mwana-kondoo** kwa hiyo sadaka, mwanangu.'"* (Mwanzo 22:7-8)




Huenda unazijua habari hizo. Mungu aliingilia kati na kutoa "***kondoo mume ....badala ya mwanawe.** Ibrahimu akapaita mahali hapo **Yehova-yire,** kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa BWANA itapatikana."* (Mwanzo 22:13-14) Kwa kuuita mlima ***"itapatikana"*** badala ya "*imepatikana*" Ibrahimu alikuwa akiitabiri siku ya maana sana ambapo Masihi ***"Mwana-kondoo wa Mungu"*** angemwaga damu yake kwenye safu ile ile ya milima kama Sadaka ya Mwisho kwa ajili ya dhambi, si kumkomboa mtu mmoja pekee, bali kutoa komboleo la mara moja tu kwa ajili ya ulimwengu, ***"**ili **kila mtu amawaminiye** asipotee, bali awe na uzima wa milele."* (Yohana 1:29; 3:16)

## Amri Kumi

Mungu aliitunza ahadi yake kwa Ibrahimu kwa kuufanya uzao wake uwe *"taifa kubwa"* – si katika *ukubwa* bali katika *umaarufu.* Mungu alikusudia kulitumia taifa hili kuyafundisha mataifa yote yajue alivyo na wenye dhambi wanavyoweza kukubaliwa naye. Wakati wa Musa, Mungu alitoa amri kumi (Kutoka 20), akitangaza, *"na alaaniwe asiyeyaweka imara maneno ya torati hii."*(Kumbukumbu 27:26)

Dhambi humtenganisha mwanadamu na Mungu. BWANA, aliye mtakatifu, hutaka utii mkamilifu.




*"Maana mtu awaye Yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote."* (Yakobo 2:10)

Bila kujali wema unaodhani kuwa nao, huwezi kufikia kiwango cha ukamilifu wa Mungu. Kama *kioo* kinachoonyesha uchafu kwenye uso wako, lakini hakiwezi kuusafisha, Sheria ya Mungu huiweka wazi dhambi moyoni mwako, lakini haiwezi kuiondoa. Amri kumi hutufundisha kuwa sisi ni **wenye dhambi tusio na msaada** na kuwa tunahitaji **Mwokozi.**

Kwa kuwa taifa lote lilikuwa na hatia kwa kuvunja sheria zake, Mungu alimwamuru Musa, *"Utanifanyia madhababu........nawe utatoa dhabihu zako juu yake."* (Kutoka 20:24) *Ni **sheria ya sadaka pekee*** ambayo ingeweza kuitangua ***sheria ya dhambi na mauti.*** Kwa njia ya sadaka ya mnyama asiye na dosari Mungu aliiadhibu dhambi bila ya kumwadhibu mwenye dhambi. Ilibidi wanaoabudu dume lenye afya njema la ng`ombe, mbuzi, mwana-kondoo au njiwa. Walionyesha imani kwenye njia ya Mungu ya haki na huruma kwa kuweka mkono kwenye kichwa cha Mnyama. Mbele za Mungu, dhambi zao zilihamishiwa kwa yule mnyama, ambaye aliuawa badala yao.



***"Kwa kuwa uhai wa mwili u katika hiyo damu;*** *nami nimewapa ninyi hiyo damu juu ya madhabahu, ili kufanya **upatanisho** kwa sababu ya nafsi."* (Walawi 17:11, Torati)

**Upatanisho** maana yake ni *kufunika.* Damu ya mnyama asiye na dosari ingeweza *kuifunika* dhambi, lakini haingeweza *kuiondoa. "Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi"* (Waebrania 10:4) Wanyama hawakuumbwa kwa mfano wa Mungu. Ni *"Mwana-kondoo"* asiye na dhambi pekee (Isaya 53:7) ambaye angeweza kuondoa deni la dhambi ya mwanadamu milele.

## Unabii zaidi

Kufuatia wakati wa nabii Musa, Mungu aliwachagua na kuwavuvia manabii wengi zaidi kutabiri, kwa kina zaidi, ujio wa Masihi *"atakayewaokoa watu wake na dhambi zao."* (Mathayo 1:21) Hapa kuna mifano michache ya unabii:

*"**Tazama, bikira atachukua mimba**, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli."* (*Imanueli maana yake ni* ***Mungu pamoja nasi***). – Isaya 7:14 (700 k. K.)

*"Bali wewe, **Bethlehemu**......kutoka kwako wewe atanitokea mmoja.....; **ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele.**"* – Mika 5:2 (700 k. K.)

***"Mungu wenu atakuja.......kuwaokoa ninyi.*** *Ndipo macho ya **vipofu** yatafumbuliwa, na masikio ya **viziwi** yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye **kilema** ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye **bubu** utaimba".* Isaya 35:4-6 (700 k. K.)

***"Wamenizua mikono na miguu"*** - Daudi, Zaburi22:16 (1000 k. K.)

*"Kama **mwana-kondoo** apelekwaye machinjioni......**Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu."*** – Isaya 53: 7, 5 (700 k. K.)

Baada ya maelfu ya miaka ya maandalizi, wakati wa Mungu ulifika wa kumtuma Masihi ulimwenguni. Lakini angekuwa *nani*? Na *angekujaje*? Kama ilivyotabiriwa na manabii, Angezaliwa na bikira kutoka kwenye ukoo wa Ibrahimu na Mfalme Daudi. Mwokozi wa wenye dhambi angetungiwa mimba kwa njia isiyo ya kurithi asili ya dhambi ya Adamu. Awe uzao wa kipekee wa mwanamke.

*"Malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi; na jina lake bikira huyo ni Mariamu......Malaika akamwambia, `Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; na jina lake utamwita* ***Yesu****. Huyo atakuwa mkuu, ataitwa* ***Mwana wa Aliye juu.****' Mariamu akamwambia malaika, `Litakuwaje neno hili maana sijui mume?' Malaika akajibu akamwambia,* ***`Roho Mtakatifu*** *atakujilia juu yako, na nguvu zake* ***Aliye Juu*** *zitakufunia kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa* ***Kitakatifu, Mwana wa Mungu…kwa kuwa hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu****."* (Injili ya Luka* 1:26-37)

*Kwenye sehemu ya pili ya Kitabu Chake (Agano Jipya), Mungu aliwavuvia Mathayo, Marko, Luka, na Yohana kuandika masimulizi ya injili kuhusu Yesu. Mungu wa pekee wa kweli hufurahia kuthibitisha kweli yake kwa mahahidi wawili.


## Mwana wa Mungu

Yule Masihi aliitwa jina lake ***Yesu,*** maana yake, *BWANA huokoa.* Na cheo chake kilikuwaje? Tusikilize tena maneno ya Gabrieli kwa Mariamu: *“Kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu,* ***Mwana wa Mungu.”***

Mungu anataka watu wote wa kila taifa waamini kuwa Yesu ni ***Mwana wake.*** Hata hivyo walio wengi hukataa kufanya hivyo. Wengi hufikiri cheo cha *“Mwana wa Mungu”* huonyesha kuwa Mungu alioa na kuzaa mwana! Biblia haifundishi hivyo.

Mwaka wa 1984, raia mashuhuri wa Senegal alikufa kwa ajali ya gari. Gazeti la taifa lilimsifu mwislamu huyu kama “mwana mashuhuri wa Senegal.” Maneno haya yalionyesha kuwa nchi hiyo ilioa na kuzaa mwana? Hapana! Waislamu wa Senegal hawana tatizo kumheshimu kwa jina hilo raia mashuhuri. Wanaelewa maana ya “mwana wa Senegal” Pia wanajua *isiyo* maana yake.

Kadhalika, Mungu mwenye enzi anapomwita Masihi ***Mwana wake*** inabidi tujue maana yake na *isiyo* maana yake. Tusidhihaki vyeo na misemo anayotukuza Muumba wetu.



Kwenye Maandiko, Masihi ana majina na vyeo zaidi ya 300. Kila usemi hutoa ufahamu mpya wa yeye ni nani na kwa nini alikuja. Kwa mfano, cheo chake cha *"Mwana wa Mungu,"* hutangaza *Ukuu wake* kama aliyetoka mbinguni. Lakini pia anaitwa *"Mwana wa Adamu,"* cheo kinachoonyesha *Unyenyekevu wake* kama aliyechagua kuzaliwa kwenye jamii yetu ya wanadamu wenye dhambi.

***"Kwa maana Mwana wa Adamu*** *hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.....**Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu,** wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake."* (Marko 10:45; Yohana 15:13)

Kama *Mwana wa Mungu* huweka mkono kwenye uungu, lakini kama *Mwana wa Adamu* huweka mkono kwenye ubinadamu. Masihi ndiye pekee *"Mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu"* (1Timotheo 2:5) anayeweza kuridhisha dai la Mungu kwa ajili ya haki na hitaji la wanadamu la rehema.

Wanaoona Masihi kuwa mwanadamu ni "chini ya ukuu wa Mungu" hawaangalii asili yake na mpango wake. Muumbaji wako, ambaye hakuona ni "chini ya ukuu wa Mungu" kutembea na kuzungumza na Adamu na Hawa, alichagua kuishi na wazazi wetu walioanguka ili awakomboe wao – na wewe na mimi – kutoka shetani, dhambi, na kifo. ***"Mungu ni upendo."*** (1Yohana 4:8)

**Mwokozi**

Kama ilivyotabiriwa na manabii, Masihi angezaliwa Bethlehemu. Lakini Mariamu aliishi Nazareti. Hili halikuwa tatizo kwa Mungu. Wakati ulipotimia, mfalme wa Kirumi alitoa tangazo akiwataka wote kurudi kwenye miji walikozaliwa wakahesabiwe kwa ajili ya kodi. Kwa hiyo Mariamu na Yusufu walisafiri kuelekea kusini hadi Bethlehemu.



*"Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia, akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng`ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.*

*Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. Malaika wa Bwana akawatokea ghafla, utukufu wa Bwana ukawang`aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akawaambia, `msiogope; kwa kuwa mimi* ***ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote;*** *maana leo katika mji wa Daudi* ***amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana!'*** *Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema, `Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu.......'"* (Luka 2:7-11, 13-14)

Kwa hiyo alikuwa nani huyu mtoto wa kiume kwenye hori na akatangazwa na malaika? Sikia tena maneno ya malaika kwa wachungaji: *"Ndiye Kristo* ***Bwana!****"




*"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu,* ***naye Neno alikuwa Mungu.*** *Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; .....Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayonuru yangaa gizani, wala giza halikuiweza.........* ***Naye Neno alifanyika mwili,*** *akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli."*

(Yohana 1:1-5, 14)

Mtu pekee aliyewahi kuzaliwa bila baba binadamu ni ***Neno****, ambaye kupitia yeye ulimwengu uliumbwa. Yeye ndiye *Uzao wa mwanamke* ulioahidiwa na Mungu siku ile dhambi ilipoingia kwa binadamu. Yeye ndiye ***"Mwana-kondoo wa Mungu*** *aichukuaye dhambi ya ulimwengu."*
(Nabii Yohana [Yahya]; Yohana 1:29)

*Kristo ni neno la Kigriki lenye maana ya Masihi, yaani *Mpakwa mafuta.* Na Bwana ndiye BWANA!
*Pamoja na Kurani nayo kumwita Yesu *Neno la Mungu* (Kiarabu: *Kalimat Allah;* Sura 3:45; 4:171), lakini hukipa cheo hiki maana tofauti. Kurani pia humwita Yesu *Masihi* na *Roho itokayo kwa Mungu* (4:171).

## Matendo ya Miujiza




Kama shetani alivyo mjaribu Adamu, pia alijaribu kumshawishi Yesu atende dhambi. Lakini tofauti na Adamu, Yesu hakujikabidhi kwa shetani. Tangu utoto hadi ukubwani, Bwana Yesu alizitii Amri Kumi na sheria zote za Mungu kikamilifu – kwa nje na kwa ndani. *"Alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote – **bila kufanya dhambi."*** (Waebrania 4:15) Kwa kuwa hakuwa na dhambi, hakustahili kufa. Lakini alikuja kwa kusudi hilo hilo.

Akiwa wa miaka 30, Yesu alianza kusafiri nje ya mji wake wa Nazareti, akifundisha na kuhubiri, akiwaita watu wa kiume na wa kike wamfuate, akitoa mapepo, akifufua wafu, akiwaponya viziwi na vipofu. Yesu alitenda miujiza hadi watu wakamjua ni nani, na kuamini. Ni nani wa kuweza kushibisha wenye njaa 5000 kwa chakula cha kijana mdogo isipokuwa Mungu? Yesu aliweza. Ni nani isipokuwa Mungu wa kuweza kutuliza dhoruba? Yesu aliweza.

Yesu aliponya kila aina ya ugonjwa. Na hakufanya hivyo kwa dawa au uchawi. Alifanya hivyo kwa kutamka. Kwa kuwa yeye *Ndiye Neno* ambaye kwa yeye ulimwengu uliumbwa, kila sehemu ya asili ilikuwa chini ya mamlaka yake. Hata hivyo, huduma ya msingi wa Masihi haikuwa kumaliza matatizo ya watu ya mwili, bali kuwaleta kwenye uhusiano sahihi na Mungu.


*"Wakamletea mtu mwenye kupooza, amelala kitandani; naye Yesu, alipoiona imani yao, alimwambia yule mwenye kupooza, `**Jipe moyo mkuu, mwanangu; umesamehewa dhambi zako.'** Na tazama**,** baadhi ya waandishi wakasema nafsini mwao, `Huyu anakufuru'. Naye Yesu, **hali akijua mawazo yao,** akasema, `Mbona mnawaza maovu mioyoni mwenu? Kwa maana rahisi ni lipi, ni kusema, "Umesamehewa dhambi zako", au ni kusema, "Ondoka, uende"? Lakini **mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi.....',** (amwambia yule mwenye kupooza), `**Ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani kwako` Akaondoka, akaenda zake nyumbani kwake.** [8]Makuhani walipomwona, walishikwa na hofu"* (Mathayo 9: 2 – 8)

Hakuna aliyewahi kutamka maneno kama ya Yesu. Kwa mfano, alifundisha, *"Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; Mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi."* (Yohana 14:6) Yesu ni tofauti na viongozi wa dini wanaosema, "Fanya hivi! Usifanye vile! Fuata sheria hizi. Hii ndiyo njia." Yesu alisema tu, ***"MIMI NDIMI** Njia."* Yesu alisema tu, ***MIMI NDIMI** huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi, "* kisha akamwita maiti aliyekuwa kaburini siku nne akarudia uhai (Yohana 11:25- -). Matendo yake yalithibitisha maneno yake kuwa ya kweli.

## Nuru

Yesu pia alisema, ***"Mimi ndimi nuru ya ulimwengu,*** *yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima."* (Yohana 8:12)

Manabii walikuwa kama mwezi, wakionyesha sehemu kidogo tu ya nuru ya Mungu kwenye ulimwengu wa giza. Lakini kwenye Maandiko ya manabii, masihi huitwa ***"Jua*** *la haki"* na "***Mwangaza*** *utokao juu."* (Nabii Malaki 4:2; Nabii Zekaria, Luka 1:78) Yesu ni "***Nuru*** *ya ulimwengu,"* ndiye chanzo cha nuru na uzima. Utukufu ulioangazia ulimwengu siku ya kwanza ya uumbaji ulikuwa umefichwa ndani ya Yesu! Alikuja kuliondoa giza la dhambi aturudishe kwa Mungu.



Muda mfupi kabla ya Yesu kuutoa mwenyewe uhai wake, alichagua mashahidi watatu, "*akawaleta juu ya mlima mrefu .....; akageuka sura yake mbele yao; uso wake ukang`ara kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru.......wingu jeupe likawatia uvuli, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, `**Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye!*** (Mathayo 17:1-2, 5)


Ni Yesu pekee aliyejua kabisa
lini angekufa,
wapi angefia,
angekufaje,
na kwa nini.

Wakati ukikaribia wa yeye kuteswa na kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu za zamani, za sasa na zijazo, Yesu aliwaambia wafuasi wake, *"Tazameni, tunapanda kwenda Yerusalemu, na* ***mambo yote yatatimizwa, Mwana wa Adamu aliyoandikiwa na manabii.*** *Kwa kuwa atatiwa mikononi mwa mataifa, atafanyiwa dhihaka**,** atatendewa jeuri**,** na kutemewa mate; nao watampiga mijeredi, kisha* ***watamwua.*** *Na* ***siku ya tatu atafufuka."*** (Luka 18:31-33)

Viongozi wa kidini walimchukia Yesu *"kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu."* (Yohana 19:7) Lakini kilichowasumbua zaidi ni kuwa watu wengi sasa walimsikiliza *yeye* kuliko *wao*! Hivyo waliunda njama ya kumwua, wasijue kuwa wanatimiza Maandiko ya manabii: kuwa Masihi ange*"dharauliwa na kukataliwa na watu"* kisha apelekwe *"kama mwana-kondoo apelekwaye machinjioni."* (Isaya 53:3, 7)


## Sadaka ya mwisho

Hivyo Bwana Yesu aliruhusu yeye mwenyewe akamatwe, ahukumiwe, adhihakiwe, avikwe taji ya miiba, apigwe mijeredi, avuliwe nguo, na kupigiliwa misumari akiwa kwenye msalaba wa mbao kwenye safu ile ile ya milima ambako miaka 2000 ya nyuma Ibrahimu alitabiri, ***"Mungu atajipatiia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka."*** (Mwanzo 22:8) Mungu alimwachilia mwana wa Ibrahimu lakini haku***"mwachilia Mwana wake mwenyewe"*** (Warumi 8:32)



Unabii wa Ibrahimu ukawa wa kweli. *Mungu alimtoa* ***Mwana-kondoo*** *– Mbadala Mkamilifu.* Yesu alipoichukua adhabu tunayostahili mimi na wewe, Mungu huko mbinguni aliifunika dunia kwenye giza. Yesu kwa hiari yake aliibeba dhambi na aibu yetu. Bwana Yesu asiye na dhambi aliibeba hukumu ya Mungu juu ya dhambi ili tuweze kuwekwa huru kutoka kwenye *sheria ya dhambi na mauti.* Pamoja na uungu wake, Yesu aliistahimili hukumu yetu kwa wakati ili tusiikabili hukumu ya milele. Na kabla tu ya kufa kwake alisema ***"Imekwisha!'*** (Yohana 19:30)


Yesu ***alilipa kikamilifu*** deni la dhambi ya ulimwengu! Hazitahitajika wala kukubaliwa sadaka zaidi kwa ajili ya dhambi. Kama kondoo wa Ibrahimu alivyokufa kwa ajili ya mmoja, Mwana-kondoo wa Mungu alikufa kwa ajili ya wote.



Yesu alikufa. Mwili wake ukaondolewa kwenye msalaba, ukafungwa kwenye kitani safi, na kulazwa kwenye kaburi. Jiwe kubwa kwenye mlango wake lilitiwa muhuri. *Kisha ikaja siku ya tatu,* ilikuwa jumapili.

Asubuhi na mapema, wanawake kadhaa waliokuwa wanafunzi watiifu wa Yesu walifika kaburini. Wakakuta jiwe limevingirishwa na kaburi likiwa tupu! Zilibaki tu zile nguo za kitani.

Malaika aliwatokea wale wanawake na kusema,*"Msiogope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa.* ***Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema.*** *Njoni, mpatazame mahali alipolazwa. Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake,* ***Amefufuka katika wafu****. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya; ndiko mtakakomwona!"* (Mathayo 28:5-7)



Hao wanawake walipokuwa wakiharakisha kwenda kuwaambia wanafunzi, Yesu alikutana nao, *"Wakakaribia wakamshika miguu, wakamsujudia."* (Mathayo 28: 9)

## Mauti Imeshindwa

Yesu alifanya asichoweza kufanya ye yote wa wahenga wetu: *Alimshinda shetani, dhambi na mauti!* Yesu alisema asichoweza kusema nabii ye yote: *"Mimi ni wa kwanza na wa mwisho, na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele! Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu."* (Ufunuo 1:17-18) Kwa kuwa Yesu aliyashinda mauti, wanaomtumaini hawana cha kuogopa katika maisha haya au yajayo.

Baada ya kufufuka Yesu alikuwa na wanafunzi wake siku 40. Aliwasaidia kuyaelewa Maandiko, akiwaonyesha kuwa manabii (Ibrahimu, Musa, Daudi n.k.) walitabiri atakavyokufa na kufufuka Masihi. Pia aliahidi kumtuma Roho Mtakatifu wake aishi ndani yao, awabadilishe wafanane na tabia yake na wawe na nguvu ya kulitangazia kila taifa Habari yake njema. Wote *wanaotubu* (wanaobadilika mawazo na mwelekeo) na *kumwamini* Mwana-kondoo wa Mungu aliye mkamilifu, aliyekufa badala yao na kuyashinda mauti, watasamehewa, watahesabiwa haki, na kuletwa kwenye uhusiano na Mungu.



Siku ya arobaini, wanafunzi wake walipokuwa wakiangalia, Yesu alipaa mawinguni hadi kwenye makao ya Baba, akiahidi kurudi mwisho wa dahari, kama mhukumu wa dunia yote. Lakini hiyo ni habari nyingine!

Tulianza kwa kuuliza kama unayajua majina ya wahenga wako waliopita. Kama unayajua au la, thamani yake ni ndogo. Lakini kuna jina alilolitangaza Mungu kuwa lenye thamani isiyopimika; jina linaloweza kubadilisha maisha yako sasa na milele.

Jina hilo ni ***YESU*** – jina lenye maana ya *BWANA huokoa.*

*"Huyo **Manabii wote** humshuhudia, ya kwamba **kwa jina lake** kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi. **Kwa jina la Yesu Kristo**. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana **hapana jina jingine** chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."* (Matendo 10:43; 4:10, 12) *Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili **mjue** ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini **Jina la Mwana wa Mungu."*** (1Yohana 5:13)

Ndiyo, unaweza **kujua** utakuwa wapi milele. Muumbaji wako anakukaribisha umwamini; uruhusu *Habari Zake* zizifanyie mageuzi *habari zako.* Kama utahamisha tumaini lako *kutoka* kujitumainia mwenyewe na dini yako, *ukalihamishia* kwa Bwana Yesu Kristo na alichofanya kwa ajili yako kwa kufa na kufufuka kwake, basi anakuambia na wewe binafsi: *"Amin, amin, **nawaambia,** Yeye **alisikiaye** neno langu na **kumwamini** yeye aliyenituma **yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni**, bali amepita **kutoka mautini kuingia uzimani**."* (Yohana 5:24)

## Tatizo la Mwanadamu

Adamu na Hawa walipomwasi Muumba wao, walijisababishia dhambi, na aibu.

- **Dhambi** yao iliwapeleka mafichoni.
- **Aibu** yao iliwafanya wafunike uchi wao.



*Katika haki yake,* Mungu aliyakataa mavazi yao ya majani ya mtini, lakini *katika rehema yake,* aliwavika ngozi za wanyama waliotolewa sadaka. Damu ya mnyama ilikuwa mfano wa kitu cha lazima kusafisha **dhambi** yao, na zile ngozi za wanyama zilikuwa mfano wa kitu cha lazima kufunika **aibu** yao.

Tunashiriki dhambi na aibu ya wahenga wetu. Kama wenye dhambi tunapungukiwa na kiwango cha Mungu cha haki na kwa aibu hatufai kuishi kwenye uwepo wake mtakatifu. Tunahitaji kupata msamaha wake na ukamilifu wake. Lakini tutaupataje?


- Unawezaje kusafishwa kutoka kwenye **dhambi** inayokutenganisha na Muumba wako aliye mkamilifu katika haki?
- Utahesabiwaje haki na Mungu ili uweze kuishi bila **aibu** kwenye uwepo wake milele?

Msalabani, Yesu Kristo aliteseka kwa ajili ya **dhambi yako** na kuistahimili **aibu yako.** Lakini kwa sababu hakuwa na dhambi, mauti haikuweza kumzuia abaki kaburini. Kwa kufa na kufufuka kwake anajitolea sasa *kukusafisha* na *kukuvika* – ubadilishane ***dhambi zako*** kwa ***haki yake.*** Lakini lazima uyaamini Maandiko ya Mungu. Unayaamini?



*"Ni nani **aliyesadiki** habari tuliyoileta?.......Alijeruhiwa kwa makosa yetu……Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; **Na BWANA ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote.** Nitafurahi sana katika BWANA, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; maana amenivika mavazi ya wokovu, **amenifunika vazi la haki."*** (Isaya 53: 1, 5-6; 61:10)

*"Kwa (injili) hiyo mnaokolewa; …..ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu **kama yanenavyo maandiko;** na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, **kama yanenavyo maandiko."*** (1Wakorintho 15:2-4)



- *Unafikiri* nini juu ya Yesu?
- *Unaamini* nini kuhusu maisha yake, kifo chake, kuzikwa na kufufuka kwake?
- *Habari zake* zinaleta matokeo gani kwenye *habari zako?*

# Azimio

*"Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana,na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Mtu awaye yote atakayeliita jina la BWANA ataponywa."*

(Warumi 10:9, 13; Nabii Yoeli 2:32)

**Kwa hisani ya:**

**HAMASA YA MILELE**
S.L.P. 11795,
Arusha, Tanzania
0767-288.053, 0784-288.053
hymilele@gmail.com

**LIFE CHALLENGE**
Box 50770-00200,
Nairobi, Kenya
0728-858.333
coast@lifechallenge.de